# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 23 Mei, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### DUA

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)* kwa Mwaka 2012 *(The Annual Report and Accounts of Energy and Water Regulatory Authority for the Year 2012).*

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU NA HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 153(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013.

KWA KUWA jana tarehe 22 Mei, 2013, Mheshimiwa Spika, alilazimika kuahirisha Mjadala wa Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini, kufuatia vurugu zilizokuwa zikiendelea katika Mkoa wa Mtwara.

NA KWA KUWA baada ya kuahirisha mjadala huo, Kamati ya Uongozi ya Bunge ilikutana na kukubaliana kuwa leo tarehe 23 Mei, 2013, Serikali itoe taarifa juu ya kinachoendelea kwenye Mkoa huo na hatua muhimu zinazochukuliwa na Serikali, ili kurejesha amani na kutatua matatizo yanayoendelea.

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 38(iv) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 Waziri Mkuu anaweza kutumia kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma, kwa muda usiozidi dakika kumi.

NA KWA KUWA muda huo wa dakika kumi ni mdogo sana katika kutoa taarifa ya jambo hili.

NA KWA KUWA ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kupata muda wa kutosha wa kutoa taarifa juu ya jambo hili. Ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 38(iv) ya Kanuni za Bunge Toleo na 2013, kwa mujibu wa Kanuni ya 153(i).

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Moja. Kanuni ya 38(iv) itatenguliwa kama hivi ifuatavyo:-

Kanuni ya 38(iv) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Waziri Mkuu anaweza kutumia kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, kutoa taarifa au ufafanuzi, kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi ya umma kwa muda usiozidi dakika kumi, itenguliwe na badala yake Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe taarifa hiyo kwa kutumia muda wote wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu hadi atakapomaliza kutoa taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni zilizotajwa)*

**SPIKA:** Bunge limeafikia, kanuni imetenguliwa. Sasa namwomba Waziri Mkuu atoe taarifa husika. Mheshimiwa Waziri Mkuu! Kwa niaba yake itatolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

## TAARIFA KUHUSU VURUGU ZILIZOTOKEA MTWARA

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(i) cha Kanuni ya kudumu ya Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwaasilisha Taarifa ya kuhusu vurugu zilizotokea Mtwara tarehe 22 Mei, 2013 kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 22 Mei, 2013, kulitokea vurugu kubwa katika Manispaa ya Mtwara na viunga vyake. Kiini cha vurugu hizi, ni madai ya baadhi ya wananchi wa Mtwara kupinga usafirishwaji wa rasilimali gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam. Ambapo tarehe 15 Mei, 2013 kikundi cha watu ambao hawakufahamika, walisambaza vipeperushi vyenye lengo la kuhimiza wakazi wa Mtwara kuwa siku ya Ijumaa tarehe 17 Mei, 2013, majira ya saa tatu asubuhi, wasikilize hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, ikisomwa Bungeni, ili kujua mustakabali wa gesi kutosafirishwa kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, vipeperushi hivyo, vilihimiza huduma zote za kijamii zisimamishwe siku hiyo. Pamoja na vipeperushi hivyo tarehe 17 Mei, 2013, huduma zote za kijamii

kama vile usafiri wa magari, pikipiki na baadhi ya Bajaji zilifanya kazi wakati huduma za maduka na migahawa zilifungwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini haikusomwa Bungeni siku hiyo, kikundi hicho kiliendelea kuhamasisha kwa kutumia mitandao ya Simu na karatasi za vipeperushi na kuwahimiza wananchi wasikilize hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini pindi itakaposomwa.

Mheshimiwa Spika, matukio hayo yaliendelea tena tarehe 22 Mei, 2013. Ambapo majira ya saa nne asubuhi, makundi ya vijana waliokuwa wanasikiliza Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, waliokuwa maeneo ya Sokoni, Magomeni na Mkanaredi, walipanga mawe makubwa, magogo na kuchoma moto matairi barabarani. Hali iliendelea kusambaa maeneo mengine ya mji kama vile Chuno, Chikongola, Mikindani na kutoka nje ya mji hadi Mpapura umbali wa kilomita 40 kutoka Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi, lilikabiliana na hali hiyo ya vurugu kwa kurudisha katika hali ya kawaida ya usalama pamoja na kuondosha magogo na mawe yaliyokuwa yamepangwa barabarani.

Mheshimiwa Spika, athari zilizotokana na vurugu hizo; madhara mbalimbali yamesababishwa na vurugu hizo kama hivi ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Hasnain Mohammed Murji, iliyopo Mikindani imeharibiwa na kuibiwa vitu mbalimbali.

(ii) Ofisi ya Mahakama ya Mwanzo ya Mitengo, imechomwa na kuteketea pamoja na nyaraka za ofisi.

(iii) Ofisi ya Chama cha Mapinduzi, Kata ya Chikongola, imechomwa moto.

(iv) Nyumba binafsi ya Afisa Mtendaji, Kata ya Magomeni imechomwa moto.

(v) Nyumba za Askari Polisi wanne zimevunjwa na kuibiwa vitu mbalimbali.

(vi) Nyumba ya Mwandishi wa Habari wa *TBC*, Ndugu Kassim Likongolo, imechomwa moto na kuteketea.

(vii) Ofisi ya Kata ya Chikongola, imeharibiwa na kuibiwa vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, thamani halisi ya mali zote zilizoungua na kuharibiwa bado haijapatikana. Mpaka sasa mtu mmoja Karim Shaibu, amefariki dunia katika vurugu hizo. Aidha, Askari wawili walijeruhiwa kwa bomu la kishindo.

Mheshimiwa Spika, katika *operation* iliyofanywa na Jeshi la Polisi, kukabiliana na vurugu hizo, watuhumiwa 91 wamekamatwa kwa makosa ya kufanya mikusanyiko isiyo halali na uharibifu wa mali na miundombinu. Hata hivyo, vurugu hizo zimedhibitiwa na *operation* ya kuhakikisha hali ya usalama inarejea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na usalama kuzorota kama nilivyoeleza hapo awali, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, kwa mujibu wa Sheria, aliomba kwa Waziri wa Ulinzi kuongezewa nguvu kulinda raia wasio na hatia na mali zao. Waziri wa Ulinzi alikubali na kuelekeza Jeshi la Wananchi waende mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo Askari 32 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania walianza safari kutoka Nachingwea kuelekea Mtwara. Walipokuwa njiani katika eneo la Kilimahewa, gari lao lilipata ajali ambapo Askari wanne walifariki dunia na ishirini kujeruhiwa.

Askari hao wamefariki na kujeruhiwa wakati wakiwa kazini kutekeleza wajibu wa kuwalinda Watanzania wenzao,

damu yao haitamwagika bure. Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi marehemu wetu hawa na awape nafuu Askari wetu na vijana wetu waliojeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Taifa, kwapongeza na kuwashukuru Askari wetu wa Jeshi la Polisi, ambao pamoja na uchache wao, jana tarehe 22 Mei, 2013, walifanya kazi kubwa katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana walifanya kazi kubwa katika mazingira magumu ya kurejesha amani bila kuleta madhara makubwa kwa maisha ya watu. Nawapongeza Viongozi wa Mkoa na Wilaya ya Mtwara Mjini, kwa uongozi wao, wakati wa kipindi kigumu cha vurugu. Nawashukuru sana wananchi waliojiepusha na vurugu hizo na kufuata sheria bila shuruti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili la bomba la gesi limezungumzwa sana. Waziri Mkuu na baadhi ya Mawaziri wamekwenda Mtwara na Rais amelizungumzia sana. Manufaa makubwa ambayo Mtwara itayapata yamezungumzwa sana. Utaratibu wa kusafirisha kiasi kikubwa cha gesi kwa bomba ndiyo unaotumika duniani kote kwa sababu ya unafuu wa gharama na kuhakikisha ubora wake.

Mheshimiwa Spika, faida zake Kitaifa pia zimeelezwa sana, ikiwemo Taifa kuondokana kabisa na upungufu wa nishati ya umeme na umeme kupatikana kwa bei nafuu na hivyo kuhakikisha mapinduzi ya viwanda na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasaliti wa Taifaaa letu, wanajua maendeleo makubwa yatakayopatikana Mtwara na nchi yetu kutokana na gesi. Hivyo, wanatumia vibaya ufahamu wetu mdogo kuhusu gesi na kuchochea upinzani dhidi ya Mradi huu unaotarajiwa kuwakomboa wana Mtwara na Watanzania. Watanzania na wana Mtwara, lazima kwa kauli isiyoyumba, tuzikatae njama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo Taifa moja la Tanzania, ambalo maliasili zake ni za Watanzania wote. Naomba nirudie, tunalo Taifa moja la Tanzania, ambalo maliasili zake ni za Tanzania wote. Tabia inayoanza kujengeka ya kila eneo kutaka inufaike peke yake na mali za eneo hilo italigawa Taifa letu vipande, vipande.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi za Kiraia na Vyama vya Siasa kwa maslahi binafsi yasiyo na upeo mpana, vinadhani vinaweza kuunga mkono madai ya namna hii ili kuimarisha kukubalika kwao miongoni mwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatimiza wajibu wetu wa kuwakumbusha msemo wa Wahenga usemao; "Tamaa mbele mauti nyuma." Wataipasua nchi yetu, watasababisha vifo vya maelfu ya watu, watalijaza Taifa vilema na majeruhi na hawatanufaika na matokeo hayo mabaya.

Mheshimiwa Spika, vita inayofahamika kama Vita Kuu ya Afrika katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, iliyopiganwa kati ya mwaka 1998 na 2003, msingi wake ulikuwa kupigania rasimali Mashariki ya Congo. Vita hii ilisababisha vifo vya watu 5,400,000 na wengi wao wakifa kwa magonjwa na njaa. Je, huko ndiko tunakotaka kulipeleka Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, ambapo msingi wake ulikuwa kugombania rasilimali, tusiipeleke nchi yetu huko. Kila kiongozi na kila Mtanzania ajue anayo dhamana ya kuendeleza umoja wa Watanzania, kuendeleza amani na kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tofauti zetu lazima ziendelee kuzungumzwa kwa uwazi, kuheshimiana na kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi yetu. Vyombo vya dola vitaendelea kuimarisha amani na utulivu katika eneo la Mtwara ili shughuli zote ziendelee kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani vikali vurugu zilizotokea Mtwara na tunaapa kuwasaka waasisi wa vurugu hizo, ndani na nje ya Mtwara, ndani na nje ya nchi yetu. Watu waliohusika kupanga, kushawishi, kuandaa na kutekeleza vurugu hizo hawataukwepa mkono wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona bado Serikali inaendelea kufuatilia mambo haya. Tulipokutana jana jioni tarehe 22 Mei, 2013, Kamati ya Uongozi ilijadili kwa kirefu sana kuhusu suala hili na wakawa wameagiza kwamba, baada ya kuona hali imetulia kule Mtwara, Kamati yangu tena ya Uongozi itakaa na kufanya maamuzi ambayo ilitaka kufanya.

Kwa hiyo, tutakutana tena baada ya kikao hiki, ili sasa tuwe na uhakika sisi kama Wabunge tunachukua hatua gani, lakini kwa sababu ndiyo kwanza watu tumesikia na ninao wachangiaji wengi hapa. Pia hatujui sisi kauli zetu zinaweza kuwa na moto wa kiasi gani tena. Ndiyo maana tumeamua tukae Kamati ya Uongozi, tuchukue hatua, halafu tutaendelea na hatua nyingine.

Tarehe 24 Mei, 2013 tutaendelea na Wizara ya Afrika Mashariki kama ilivyo, lakini Wizara hii katika muda mfupi, kutokana na hali halisi tutaipangia siku nyingine ili tuimalize, kwa sababu Wizara kama ilivyo haina matatizo, isipokuwa hii hali halisi, ambayo waliipanga hata kabla Waziri hajasoma hotuba yake.

Kwa hiyo, naahirisha kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi. Naomba Kamati ya Uongozi tukutane.

*(Saa 3.28 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 24 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*